
DOKEZO SABILI

KWENDA KWA: WAFANYAKAZI WOTE TAFIRI MAKAO MAKUU, KYELA, DAR ES SALAAM, SOTA, MWANZA NA KIGOMA

KUTOKA KWA: AFISA UTUMISHI NA UTAWALA

TAREHE: 11/09/2017

YAH: WATUMISHI WANAOTARAJIA KUCHUKUA MIKOPO YA PPF KUPITIA SACCOS NA TAASISI NYINGINE ZA KIFEDHA

Husika na mada tajwa hapo juu.

Hivi karibuni viongozi wa TAFIRI SACCOS wamekuwa katika mchakato wa maandalizi ya utoaji wa mikopo ya PPF kwa wanachama wake.

Kwa kuwa Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu inayo mamlaka ya kupitisha maombi ya mikopo kwa watumishi wake na pia kumuingiza mtumishi husika katika makato ya kila mwezi kwa kufuata sheria na taratibu zilizopo ninapenda kuwataarifu kuwa Ofisi haitapitisha maombi ya mikopo kwa watumishi walio katika makundi yafuatayo:-

1. Watumishi ambao kuna Benki au Taasisi yoyote ya kifedha ilileta malalamiko ya kusimama kwa makato ya madeni yao kabla ya deni kuisha. Watumishi hawa walipewa muda maalum wawasiliane na Benki husika ili kupata muafaka wa masuala yao na kisha walete barua za muafaka huo kwa mwajiri (Mkurugenzi Mkuu). Hivyo kama kuna mtumishi hajatekeleza suala hili hawezi kupitishiwa maombi ya kukopa katika Taasisi yoyote.
2. Watumishi wanaodaiwa malimbikizo ya madeni mbalimbali na Taasisi kama madeni ya kodi za nyumba, 'imprest' nk. Watumishi hawa hawataruhusiwa kukopa katika Taasisi yoyote hadi pale watakapolipa madeni yao.

3. Watumishi ambao hawajaingizwa katika makato ya kila mwezi ya kodi za nyumba kutokana na salio lao kugota theluthi moja (1/3). Watumishi hawa hawataruhusiwa kukopa katika Taasisi yoyote ya fedha hadi pale watakapoingizwa katika makato ya kila mwezi ya kodi hizo.

Tunaomba watumishi waliopo katika kundi lolote kati ya yaliyotajwa hapo juu washughulikie masuala yao ili waweze kuruhusiwa kukopa katika Taasisi yoyote ya fedha ikiwemo SACCOS.

Tunawatakia utekelezaji mwema.



Jackson E. Payowela,

AFISA UTUMISHI NA UTAWALA.